



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

OMBI LA KUONESHA NIA YA UBORESHWAJI WA SEKTA YA USHIRIKISHWAJI KWA KUTOA NA KUENDESHA GARI LA MATANGAZO NA KITUO KINACHOTEMBEA CHA HUDUMA YA USHIRIKISHWAJI WA JAMII: KUMBUKUMBU NA. REQ-0000055

Ombi la kuonesha nia ya uboreshaji wa sekta ya ushirikishwaji kwa kutoa na kuendesha gari la matangazo na kituo kinachotembea cha huduma ya ushirikishwaji wa jamii.

Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) LTD (EACOP LTD) inakaribisha kampuni zenye uzoefu na weledi wa kutosha kuonesha nia ya kutoa na kuendesha gari la Matangazo ('pop-up truck') ili kusaidia utekelezaji wa uboreshaji wa sekta na shughuli za Ushirikishwaji wa Jamii katika wilaya 27 na vijiji 231 vilivyopo katika mkuza wa bomba la mafuta.

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la kusafirisha Mafuta lililofukiwa chini ya ardhi linalokatisha mipaka ya nchi mbili litakalo safirisha mafuta ghafi kwenda kwenye masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka rasi ya Chongoleani karibu na Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA

Kwa niaba ya KAMPUNI, mkandarasi atakayeteuliwa atatoa huduma ya Kulisimamia na kuendesha "gari la matangazo ya kidijitali" ambalo litalenga kukuza ushirikishwaji na ushiriki wa jamii katika ngazi ya mkoa, wilaya na kijiji katika shughuli za EACOP. Kituo cha Ushirikishwaji kinachotembea kitatumika katika shughuli zilizoorodheshwa hapa chini:

- Ushirikishwaji wa kila robo mwaka na jamii ya wagavi katika ngazi ya mkoa na wilaya (kwa mfano: warsha za wagavi, vipindi vya utoaji wa taarifa, n.k.
- Matukio ya ushirikiano na wakandarasi Wakuu wa KAMPUNI pamoja na jamii ya wafanyabiashara wenyeji.
- Kusaidia usajili wa wagavi wa ngazi ya wilaya kwenye mfumo wa LSSP, n.k.
- Kutoa mafunzo ya muda mfupi (kati ya siku 1 hadi 2) kwa jamii ya wafanyabiashara wenyeji ili kuwajengea uwezo katika utoaji wa huduma na ujuzi wa kisekta
- Shughuli za kujenga uelewa wa jamii zinazohusiana na sera ya EACOP ya usalama, afya, ulinzi n.k. pamoja na ushirikishwaji mwingine wa jamii unaohusiana na Mradi wa EACOP unaofanywa na idara mbalimbali za EACOP

Makampuni yanayohitaji yanaweza kushiriki katika wito huu kama kampuni moja moja au muungano wa Makampuni.

VICEZO MUHIMU:

Makampuni au taasisi zinazoonesha nia zinaalikwa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zifuatazo:

- Leseni ya Biashara.
- Leseni ya biashara kutoka nchi husika inayothibitisha kufanya kazi hii.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na cheti cha uthibitisho wa mlipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Inashauriwa kuwasilisha maombi ya usajili kwenye kanzi data ya EWURA ya Watoa Huduma ya Ugavi wa Ndani (LSSP) wakati wa kuonesha nia.
- Kuzingatia kanuni za watoa huduma wa ndani za mwaka 2017 na ufafanuzi wa makampuni ya ndani.
- Wasifu wa watendaji watakaohusika katika Mradi ikiwa ni pamoja na nakala za vyeti vyao, kiwango cha elimu, uzoefu na uwezo wa kutoa huduma inayohitajika.
- Uzoefu, utendaji na uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu katika kiwango kikubwa nchini Tanzania, kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho kutoka kwenye mfumo wa Usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na Viwango vya Ndani na vya Ki-Sekta vinavyotumika kwa kazi hii.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za kupinga rushwa, ufisadi, na Haki za Binadamu.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutosha kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanapaswa kutuma maombi na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe ya procurement.tz@eacop.com (ukubwa wa barua pepe usizidi **20Mb**) mnamo au kabla ya Tarehe **15 Disemba 2022** saa **11:00 jioni** saa za Afrika Mashariki (EAT). Kichwa cha Barua pepe kiwe **[REQ-0000055]**

POP-TRUCK.

Maombi yote yakuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.

Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.

Muhimu: EACOP itapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yaliyoonesha nia kulingana na EOI hii, na kisha kufanya tathmini kulingana na vigezo vya ndani vya EACOP ili kubaini makampuni yenye sifa yatakayojumuishwa kwenye orodha ya awali ya makampuni yenye vigezo. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD ina haki ya kuteua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake bila ya kutoa sababu kwa kampuni husika.